TANGAZO LA SERIKALI NA. 81 la tarehe 7/2/2025

SHERIA YA SHULE YA SHERIA TANZANIA,
(SURA YA 425)

# SHERIA NDOGO

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 27(2)(d))*

SHERIA NDOGO ZA MITIHANI NA RUFAA ZA SHULE YA SHERIA TANZANIA ZA MWAKA 2025

Jina

TS Na. 621 la 2024

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Marekebisho ya Sheria Ndogo za Mitihani na Rufaa za Shule ya Sheria Tanzania za Mwaka 2025 na zitasomwa pamoja na Sheria Ndogo za Mitihani na Rufaa za Shule ya Sheria Tanzania za Mwaka 2024 ambazo katika Sheria Ndogo hizi zitarejewa kama "Sheria Ndogo kuu".

Marekebisho ya aya ya 22

2. Sheria Ndogo kuu zinarekebishwa katika aya ya 22, kwa-

“(a) kwa kufuta neno “mitatu” popote linapoonekana katika aya hii na badala yake kuweka neno “mitano”.

(b) katika aya ndogo ya (8) kwa kufuta maneno “ataruhusiwa kuomba kurudia program” nabadala yake kuweka maneno “ataruhusiwa kuomba kusajiliwa upya”.

Nyongeza ya aya ya 22A

3. Sheria Ndogo kuu zinarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya aya ya 22 aya ifuatayo:

“Mitihani maalumu

22A.-(1) Mtahiniwa wa programu yoyote akishindwa kufanya mitihani yote ama sehemu ya mitihani kutokana na sababu za msingi, mtahiniwa huyo atawasilisha uthibitisho wa sababu za kushindwa

kwake kufanya mitihani hiyo kwa Mkuu wa Shule na endapo sababu zake zitakubalika ataruhusiwa kufanya mitihani au mtihani maalum.

(2) Mitihani Maalumu itafanyika katika vipindi vya kawaida vya mitihani au katika kipindi kingine chochote kitakachoamuliwa na Mkuu wa Shule.

(3) Mtahiniwa atakayefanya mitihani maalumu na kutakiwa kufanya mitihani ya marudio baada ya matokeo yake kutoka, atafanya mitihani ya marudio kwa kuzingatia masharti ya aya ya 22.”.

Dar es Salaam,
4 Januari, 2025

SAMWEL M. MANENO,
*Mwenyekiti wa Bodi*